**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)**

**MAREJEO YA MKATABA WA ZABUNI (KUUZA, KUTENGENEZA NA KUFUNGA MADIRISHA YA ALUMINIUM KATIKA CHUO CHA WILAYA YA BUTIAMA)**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 17 mwezi 05 2022

**KATI YA**

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA - MARA, S.L.P. 188, MUSOMA - MARA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 DODOMA (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

**NA**

TAWAQAL SEIF SAMBIRO S.L.P. 11001, MWANZA. (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni") Mtengenezaji na mfungaji wa madirisha ya Aluminium kwa upande mwingine.

**KWA KUWA** Mwajiri anasimamia mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA (BUTIAMA DVTC);

**KWA KUWA** Mwajiri amekubaliana na muuzaji, mtengenezaji na mfungaji wa madirisha ya Aluminium katika ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA(BUTIAMA DVTC);

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya makubaliano na Muuzaji, mtengenezaji na mfungaji wa madirisha ya Aluminium katika ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA(BUTIAMA DVTC);

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

1. **GHARAMA YA KUNUNUA MADIRISHA,KUTENGENEZA NA KUPACHIKA**
   Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania ***145,470,000/=(Milioni mia moja arobaini na tano, laki nne na sabini elfu)*** Mzabuni atatengeneza,kuuza na kufunga madirisha ya Aluminium katika majengo ya Mradi wa Chuo cha Wilaya ya

Butiama(BUTIAMA DVTC) kwa Idadi, vipimo na aina ya vifaa vyenye sifa tajwa hapo chini.

**"Supply and FIX the below windows with the following specifications: 100mm wide, 2mm thick bronze anodized aluminum, 6mm clear sheet grass windows complete with glazing, sliding mosquito gauze pane and all necessary iron mongery to engineer's satisfaction"**

| S/n | Item Code | Description of Supplies or Services | Unit | QTY | Unit Price | Tax per unit [VAT] | Extended Price (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (1) | (2) | (3) | (4) | (5) | (6) | (7) | (8) |
| | | | | | | | [(6+7)x5 |
| 1 | | Windows; 2000x1850mm | Complete | 18 | 700,000.00 | | 12,600,000.00 |
| 2 | | Windows; 1500x1850mm high | Complete | 4 | 660,000.00 | | 2,640,000.00 |
| 3 | | Windows; 2000x1350mm high | Complete | 1 | 660,000.00 | | 660,000.00 |
| 4 | | Windows; 1200x1350mm high | Complete | 2 | 360,000.00 | | 720,000.00 |
| 5 | | Windows; 800x1350mm high | Complete | 8 | 280,000.00 | | 2,240,000.00 |
| 6 | | Supply and fix curtain walling with aluminum spider frames sizes; 6700 x 2850mm | Complete | 1 | 3,900,000.00 | | 3,900,000.00 |
| 7 | | Windows; 3770 x 2200mm | Complete | 11 | 1,800,000.00 | | 19,800,000.00 |
| 8 | | Windows; 3770 x 1820mm | Complete | 6 | 1,200,000.00 | | 7,200,000.00 |
| 9 | | Windows; 2870 x 1820mm | Complete | 36 | 790,000.00 | | 28,440,000.00 |
| 10 | | Windows; 1000x600mm | Complete | 18 | 230,000.00 | | 4,140,000.00 |
| 11 | | Window 2000x600mm | Complete | 6 | 290,000.00 | | 1,740,000.00 |
| 12 | | Window 1600x1800mm | Complete | 1 | 680,000.00 | | 680,000.00 |
| 13 | | Window 800x950mm | Complete | 2 | 260,000.00 | | 520,000.00 |
| 14 | | Window 4770x950mm | Complete | 4 | 760,000.00 | | 3,040,000.00 |
| 15 | | Windows; 1500x1600mm | Complete | 41 | 480,000.00 | | 19,680,000.00 |
| 16 | | Windows; 2700x900mm | Complete | 4 | 500,000.00 | | 2,000,000.00 |
| 17 | | windows; 2400x900mm | Complete | 2 | 440,000.00 | | 880,000.00 |
| 18 | | Windows; 2670 x 2100mm | Complete | 3 | 800,000.00 | | 2,400,000.00 |
| 19 | | Windows; 2500 x 2100mm high | Complete | 17 | 790,000.00 | | 13,430,000.00 |
| 20 | | Windows; 2500 x 1200mm high | Complete | 2 | 680,000.00 | | 1,360,000.00 |
| 21 | | Windows; 1200 x 1200mm high | Complete | 2 | 320,000.00 | | 640,000.00 |
| 22 | | Window 1800x2100 | Complete | 4 | 700,000.00 | | 2,800,000.00 |
| 23 | | Windows; 1500x1800mm | Complete | 14 | 660,000.00 | | 9,240,000.00 |
| 24 | | Windows; 1200x1800mm | Complete | 2 | 440,000.00 | | 880,000.00 |
| 25 | | windows; 900x1800mm | Complete | 2 | 360,000.00 | | 720,000.00 |
| 26 | | Windows; 900x900mm | Complete | 4 | 310,000.00 | | 1,240,000.00 |
| 27 | | Windows; 1200x1800mm | Complete | 2 | 440,000.00 | | 880,000.00 |
| 28 | | windows; 1200x1200mm | Complete | 2 | 320,000.00 | | 640,000.00 |
| 29 | | windows; 800x600mm | Complete | 2 | 180,000.00 | | 360,000.00 |
| | | | | | | | |

| S/n | Item Code | Description of Supplies or Services | Unit | QTY | Unit Price | Tax per unit [VAT] | Extended Price (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (1) | (2) | (3) | (4) | (5) | (6) | (7) | (8) |
| TOTAL | | | | | | | 145,470,000.00 |

2. **MABADILIKO YA GHARAMA ZA MANUNUZI YA VIFAA VYA UJENZI**

Gharama ya kuuza, kutengeneza na kufunga madirisha ya Aluminium haitabadilika kwa namna yoyote ile ndani ya kipindi cha muda wa MIEZI mitatu tokea tarehe ya kufunga mkataba huu.

3. **NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

i. Mwajiri atamlipa Mzabuni kwa kutumia Mfumo wa Ulipaji Serikalini(MUSE) kwa mfumo wa mkataba ndani ya siku saba(07) mara baada ya kuanza kazi na malipo yatalipwa kwa awamu tatu.

(a) Malipo ya awamu ya kwanza 40% ya gharama yote kama malipo ya awali

(b) Malipo ya awamu ya Pili 40% ya gharama yote.

(c) Malipo ya awamu ya Tatu na ya mwisho 18% ya gharama yote mara baada ya kazi kamilisha.

(d) Withholding tax 2% ambayo ni makato yaliyopo kisheria.

4. **MAKABIDHIANO YA VIFAA VYA UJENZI**

(a) Madirisha ya Aluminium yatawasilishwa kwenye eneo la ujenzi na mzabuni kutakiwa kutoa nyaraka muhimu za vifaa husika. Vile vile pande zote mbili zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini katika daftari maalum la mapokezi.

(b) Pindi Madirisha ya Aluminium yatawasilishwa kwenye eneo la ujenzi yatakaguliwa na Kamati ya Mapokezi ili kujiridhisha vitu vifuatavyo.

i. Ubora wa vifaa
ii. Idadi ya vifaa
iii. Muda wa Ukomo wa matumzi wa vifaa
iv. Kama kuna uharibifu wowote

( c) Pindi Madirisha ya Aluminium yatapokuwa yamepokelewa Mzabuni atawajibika Kuyafunga katika sehemu zake husika.

5. **WAJIBU WA MZABUNI**

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Marejeo haya ya Mkataba ni ya siku ***Ishirini na moja*** (WIKI TATU)

(b) Kuwasilisha vifaa kwenye eneo la ujenzi ndani ya muda uliowekwa ambao ni siku Ishirini na moja(21)

(c) Kubadilisha kifaa ambacho kitakuwa kimekutwa na mapungufu na kamati ya Mapokezi na kuleta kifaa kingine ambacho kitakuwa na sifa stahiki mara baada ya kufungwa na kukaguliwa

(d) Kuuza, kutengeneza na kufunga madirisha ya Aluminium na kukabidhi kwa Afisa ugavi,Kamati ya mapokezi na msimamizi wa mradi wa chuo cha Wilaya ya Butiama.

(e) Kazi ya utengenezaji wa madirisha ya Aluminium na ufungaji unafanyika katika hali ya ubora unaohitajika.

(f) Iwapo Mwajiri atashindwa kutekeleza malipo ndani ya muda uliowekwa,Mwajiriwa atakuwa na wajibu wa kumuandikia barua mwajiri ili kumueleza changamoto ya malipo yake itayopelekea kushindwa kutekeleza wajibu wake.

6. **WAJIBU WA MWAJIRI**

Mwajiri atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kumlipa mzabuni malipo halali ya kazi iliyoainishwa katika Mkataba huu kulingana na utaratibu uliobainishwa katka kipengele Na.3 cha Mkataba huu, pale Mzabuni atakapokuwa ametimiza wajibu wake kikamilifu kulingana na Mkataba huu.

(b) Kupokea vifaa ambavyo vimekidhi vigezo vyote kwa ajili ya ujenzi.

(g) Kuhifadhi na kutekeleza masharti yote ya Sheria za nchi zinazohusiana na kazi anayoifanya Mzabuni;

(c) Kumkata Mzabuni kodi ya zuio (withholding tax).

(d) Iwapo Mwajiriwa atashindwa kutekeleza wajibu wake ndani ya muda uliowekwa,Mwajiri atakuwa na wajibu wa kumuandikia barua mwajiriwa ili kupata maelezo ya ucheleshwaji huo.

7. **MAMBO YALIYO NJE YA UWEZO WA KIBINADAMU**

Itakapotokea jambo lolote lililo nje ya uwezo wa kibinadamu kama vile mafuriko, kimbunga, tetemeko la ardhi na mambo yanayofanana na hayo, pande zote mbili zitapata nafasi ya kulijadili na kulipatia ufumbuzi wa haraka.

8. **SHERIA ZINAZOTUMIKA**

Sheria za kutafsiri Mkataba huu na ufanyaji wa kazi katika Mkataba huu ni Sheria za Tanzania.

## 9. USIRI

Nyaraka zote zitakazokuwa zimetumika katika ujenzi unaohusu Mkataba huu hazitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa ujenzi unaohusu Mkataba huu. Pia taarifa yoyote itakayopatikana wakati wa ujenzi unaohusu Mkataba huu haitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa ujenzi unaohusu Mkataba huu.

## 10. USULUHISHI WA MIGOGORO

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhisha mgogoro, basi upande wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi(arbitration).

**IMESAINIWA NA KUWEKWA MIHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA VETA-MARA**

Jina: DAVID LOUIS BENEDICT Saini: ______________

Wadhifa: MSIMAMIZI WA MRADI BUTIAMA DVTC Tarehe: 17/05/2022

MKUU WA CHUO VETA-MARA P.O.BOX 183 MUSOMA

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: ALFRED G KULIFU Saini: ______________

Wadhifa: AFISA MANUNUZI MSAIDIZI Tarehe: 17/05/2022

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: VAN -C- CHADEWA Saini: ______________

Wadhifa: SHAHIDI/MJUMBE Tarehe: 17.05.2022

**IMESAINIWA NA MZABUNI**

Jina: TAWAQAL SEIF SAMBIRO Saini: ______________

Wadhifa: DIRECTOR Tarehe: 17.05.2022

TAWAQAL SEIF SAMBIRO S.L.P 11001 MWANZA TIN: 114-777-803

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: NEEMA-S- JOHN Saini: ______________

Wadhifa: MANAGER Tarehe: 17-05-2022.